**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM**

# TAARIFA KWA UMMA

## KULAANI VITENDO DHIDI YA UDHALILISHAJI WA KIJINSIA

**Dodoma, 5 Agosti, 2024**

Kuanzia tarehe 4 Agosti, 2024 kuna video imesambaa kwenye mitandao ya kijamii ikimuonesha mwanamke anayesemekana anatoka eneo la Yombo Dovya, Jijini Dar es Salaam akifanyiwa vitendo vya udhalilishaji kinyume na sheria na maadili ya nchi.

Wizara inaungana na Jeshi la Polisi Tanzania kukemea vitendo vya unyanyasaji na udhalilishaji wa kijinsia vinavyoendelea kutokea katika jamii yetu ikiwemo mitandao ya kijamii. Aidha, nitumie fursa hii kuwasihi Wananchi wote kutofumbia macho vitendo hivi na kutoa taarifa ya matukio kama haya kwa Jeshi la Polisi Tanzania ili hatua za kisheria ziweze kuchukuliwa.

Wizara inatumia fursa hii kusisitiza wananchi kuzingatia Sheria, Mila, Miiko, Desturi na Maadili ya Mtanzania katika kushughulikia masuala mbalimbali ya mahusiano kuliko kujichukulia Sheria mkononi.

***Tanzania bila ukatili wa kijinsia, inawezekana!***

Dkt. Nandera E. Mhando
**KAMISHNA WA USTAWI WA JAMII**